**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA**

**MTIHANI WA PAMOJA WA KIDATO CHA PILI**

**021 KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:30** **MACHI 2024**

**MAELEKEZO**

1. Mtihani huu una sehemu A,B na C zenye jumla ya maswali kumi (10)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A,B na C.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali.
4. Andika kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au nyeusi.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa, Haviruhusiwi katika chumba cha mtihani.

## SEHEMU A (ALAMA 15)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu katika karatasi yako ya kujibia.

   i) Mwalimu alimuuliza Chimale maana ya lugha, Chimale alijibu kama ifuatavyo " Ni chauti za nachibu". Mwalimu alifurahi na kusema hongera kaka wa kimakonde. Unafikiri mwalimu alimwambia Chimale kaka wa kimakonde kwa sababu gani?

   A. Lafudhi
   B. Kiimbo
   C. Sauti
   D. Matamshi
   E. Mkazo

   ii) Ni aina ya neno ambalo haliwezi kusimama pamoja na nomono.

   A. Kivumishi
   B. Kielezi
   C. Kiwakilishi
   D. Kiunganishi
   E. Kitenzi

   iii) Wakati mwalimu anafundisha matawi ya sarufi, alimchagua Amina kutaja tawi la sarufi linaloshughulikia muundo wa sentensi. Amina alijibu kwa kulitaja tawi hilo la sarufi kuwa ni ;

   A. Fonolojia
   B. Semantiki
   C. Sintaksia
   D. Matamshi
   E. Maana

   iv) Warioba ni mahiri sana katika kutenganisha silabi katika maneno. Mdhihirishie na wewe kuwa mahiri wa kutenganisha silabi katika neno "Walifundishwa" kwa kumweleza kuwa lina silabi.

   A. Sita
   B. Tano
   C. Kumi na tatu
   D. Nane
   E. Tisa

   v) Katika kamusi kuna maneno yanayoandikwa kwa wino uliokolezwa. Maneno hayo hujulikana kama;

   A. Kitomeo
   B. Kidahizo
   C. Matini
   D. Sherehe
   E. Pijini

   vi) Wageni wetu walikaribishwa vizuri sana. Neno "Sana" ni aina gani ya neno

   A. Kielezi
   B. Kitenzi
   C. Kivumishi
   D. Kiwakilishi
   E. Kihisishi

   vii) Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo haina maana zaidi ya moja?

   A. Kaka amefua nguo
   B. Nipe sahani ya kulia
   C. Asha amenunua mbuzi
   D. John ameuza kanga
   E. Manula amempigia mpira.

viii) Lugha ni kama Kinyonga kwani hubadilika kulingana na mazingira na wakati. Je ni mabadiliko gani yamesababisha kuundwa kwa neno “Nywila”?

A. Mabadiliko ya kiuchumi
B. Mabadiliko ya sayansi na teknolojia
C. Mabadiliko ya utamaduni
D. Mabadiliko ya kijamii
E. Mabadiliko ya kisiasa.

ix) Kuna wakati watumiaji wa lugha hufanya makosa pasipo kukusudia. Katika sentensi “Waziri wa fedha atawakilisha bajeti yake ya mwaka 2023/2024”. Ina kosa gani la kisarufi?

A. Kosa la kimsamiati
B. Kosa la kimuundo
C. Kosa la kimatamshi
D. Kosa la kimaana
E. Kosa la kimaandishi

x) Sanaa ni ufundi wa kuwasilisha wazo lililo katika fikra za binadamu. Ni seti ipi imejumisha tawi lisilo la Sanaa?

A. Maonesho, usususi na ngoma
B. Ufinyazi, uhunzi na uchoraji
C. Fasihi, utarizi na uchonganishi
D. Muziki, ufumaji na ususi
E. Fasihi, ngonjera na nyimbo

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

**2.** **Kwa** kuzingatia uandishi wa barua ya kirafiki oanisha kauli katika orodha A kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka orodha B

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i. Mpendwa mama, shikamoo | A. Anuani ya mwandishi |
| ii. Wako mwanao mpendwa Pakome | B. Tarehe |
| iii. S.L.P 265, Masasi | C. Mwanzo wa barua |
| iv. Naomba unitumie fedha za matumizi | D. Anuani ya mwandikiwa |
| v. 10/02/2024 | E. Mwisho wa barua |
| | F. Kiini cha barua |

**MAJIBU**

| **ORODHA A** | **i** | **ii** | **iii** | **iv** | **v** |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

## SEHEMU B (ALAMA 70)

**3.** Kamusi huwa na mambo mengi ya msingi. Mambo hayo huweza kumsaidia mtu asiyejua vizuri lugha ya Kiswahili. Ukiwa mwanafunzi wa kidato cha pili, mtajie rafiki yako mambo matano ya msingi ambayo huwemo katika kamusi.

**i)** ______________________________________________________________________

**ii)** ____________________________________________

**iii)** ____________________________________________

**iv)** ____________________________________________

**v)** ____________________________________________

**4.** Vijana wa kileo hupenda sana kutumia misimu kwa kudhani ndiyo ubobezi wa lugha badala yake huathiri lugha kuu. Kwa kurejea lugha ya Kiswahili eleza athari tano (5) za kutumia misimu.

**i)** ____________________________________________

**ii)** ____________________________________________

**iii)** ____________________________________________

**iv)** ____________________________________________

**v)** ____________________________________________

**5.** Mwalimu wa Kiswahili aliwafundisha wanafunzi wa kidato cha pili mtindo wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali. Ukiwa miongoni mwa wanafunzi hao, eleza miktadha iliyotumika katika sentensi zifuatazo:

**i)** Wapendwa inabidi tumjue mungu maana mshahara wa dhambi ni mauti.____________________________________________

**ii)** Mbili asubuhi, mbili mchana na mbili jioni. ____________________________

**iii)** Kitangari, Newala, Masasi wahi hiyoooo ____________________________

**iv)** Aziz, Aziz anakwenda na mpira anapiga chenga pale goooo ____________________

**v)** Lete kama tulivyo, Nipe na konyagi moja ____________________________

**6.** Kwa kutumia mifano anuai kutoka katika lugha ya Kiswahili, eleza maana ya istilahi zifuatazo**.**

**i)** **Uambishaji ____________________________________________**

**____________________________________________**

ii) Misimu ____________________________________________

____________________________________________

iii) Lugha ____________________________________________

____________________________________________

iv) Rejesta ____________________________________________

____________________________________________

7. Eleza kazi moja ya viambishi vilivyopigiwa mstari katika maneno yafuatayo;

i) Hupenda

ii) Mtapenda

iii) Anapendwa

iv) Amependa

v) Aliyependwa

8. Ukiwa kama mwanafunzi wa kidato cha pili, eleza mambo matano (5) ya msingi ya kuzingatia unapofupisha habari.

i) ____________________________________________

ii) ____________________________________________

iii) ____________________________________________

iv) ____________________________________________

v) ____________________________________________

9. Mtangazaji wa televisheni, huhakikisha watazamaji wanapata habari sahihi kwa wakati. Katika fasihi ni mambo gani msanii huzingatia anapowasilisha maudhui katika jamii?

i) ______________________________________________________________________

ii) ______________________________________________________________________

iii) ______________________________________________________________________

iv) ______________________________________________________________________

v) ______________________________________________________________________

SEHEMU C (ALAMA 15)

10. Mwalimu Makoye hapendi michezo, kila mara amekua akiwakataza wanafunzi wake kucheza michezo mbalimbali kwani itawafanya wapoteze muda wao hivyo kufeli katika mitihani yao. Ukiwa mwanafunzi wa kidato cha pili, eleza hoja tano (5) za kumshawishi mwalimu Makoye awaruhusu kucheza michezo shuleni.